

TANGAZO LA KOZI NA UDHAMINI

HAIRSTYLING CERTIFICATION

& BUSINESS EDUCATION

Nafasi Opportunity Society (NOS) ni taasisi iliyoko nchini Canada inayosaidia wasichana wa Kitanzania kwa kuwapatia ujuzi ili kujikomboa na umasikini.

Katika mwaka wa 2014 NOS itatoa udhamini kwa wasichana 25 kwa kuwalipia ada na fedha ya kujikimu ili kupata mafunzo ya "Hairstyling and Business Skills"

Mafunzo yatatolewa kuanzia **Novemba 2014** mpaka **Mei 2015** jijini Dar es Salaam kwa ushirikiano na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kozi itahusisha nadharia na vitendo katika Shule ya Urembo.

Sifa za Mwombaji:

- Awe msichana wa Kitanzania wa umri wa kati ya miaka 18 – 28.
- Awe amehitimu elimu ya Kidato cha Nne au Zaidi.
- Awe na ufahamu wa awali wa Lugha ya Kiingereza.
- Awe na shauku/ari ya kujifunza mambo ya urembo.
- Awe ametoka katika familia isiyo na uwezo kiuchumi.

Jinsi ya Kutuma Maombi:

Fomu za maombi zinapatikana katika ofisi za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania zilizoko;

1. Kinondoni Makao Makuu (Block C, Ground Floor ICE office, ulizia Mr Muda)
2. Kinondoni Regional Centre (karibu na Kiwanja cha Biafra, ulizia Mr. Adrian)
3. Temeke Regional Centre (ndani ya viwanja vya Sabasaba, ulizia Mr. Ben Mwinuka)

4. Ilala Regional Centre (Jengo la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, ulizia Ms Martha Kabate)

Fomu zilizojazwa ziambatanishwe na

- Vyeti vya elimu ya Sekondari
- Nakala (**photocopy**) ya kitambulisho chochote kinachokubaliwa na Serikali kama vile, Kitambulisho cha Mpiga Kura, Kitambulisho cha Taifa, cheti cha kuzaliwa n.k.
- Picha ndogo ya rangi (passport size)

Zitumwe Kwa:

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Nafasi Opportunity Scholarship Committee,
Kawawa Road, Kinondoni Municipality,
P. O. Box 23409,
Dar es Salaam

Au zirudishwe moja kwa moja kwenye moja ya Ofisi za Chuo zilizotajwa hapo juu

NB: *Maombi yatumwe kabla ya Oktoba 27, 2014*

Waombaji watakaoorodheshwa wataitwa kwa usaili

Kwa Maelezo Zaidi Wasiliana Na:

Program Coordinator:

Simu: 0767-971015
Barua pepe: krwegasira@gmail.com.

